

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU DHAMIRA YA SERIKALI YA KUTEKELEZA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE

Dodoma, 27 Septemba, 2022

Ndugu Wanahabari,

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wananchi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya karibu na maeneo yao kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa wa ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini.

Tangu na baada ya uhuru mwaka 1961, Serikali imekua ikitekeleza afua mbalimbali kwa lengo la kupambana na maadui wakuu watatu (3) wa maendeleo ambao ni ujinga, maradhi na umaskini. Katika kupambana na adui maradhi, Serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali ikiwemo kutunga

na kutekeleza Sera, Miongozo na Sheria yenye lengo la kuboresha na kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya nchini.

Ndugu Wanahabari,

Kutokana na jitihada hizo na kwa uongozi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwa ni pamoja **kuongezeka kwa idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 6,871 mwaka 2015/16 hadi kufikia 10,380 mwaka 2021/22**, Watumishi wa Sekta ya Afya wameongezeka kutoka 86,152 mwaka 2015/16 hadi 102,469 mwaka 2021/22, **Bajeti ya dawa na vitendanishi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 30 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi bilioni 230 mwaka 2022/23.**

Ili kuimarisha na kusogeza upatikanaji wa huduma za vipimo vya kibingwa ngazi ya Mikoa, Serikali inaendelea kusambaza na kusimika mashine za kisasa za CT-Scan katika hospitali ngazi ya Taifa, Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa ishirini na nane (28).

Ndugu Wanahabari,

Katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata huduma bora za afya, Wizara imefanya mapitio ya mwongozo wa matibabu nchini na Orodha ya Taifa ya dawa muhimu (STG/NEMLIT) ili kuhakikisha watoa huduma wote wanatoa huduma bora kwa wananchi kwa kuzingatia miongozo iliyowekwa na Wizara.

Aidha, katika kuimarisha upatikanaji, usambazaji na utunzaji wa dawa, Serikali imefanya maboresho makubwa katika uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi.

Ndugu Wanahabari,

Pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali za kuimarisha upatikanaji na utoaji huduma za afya nchini, bado kumekuwepo changamoto kwa baadhi ya wananchi kushindwa kugharamia uchangiaji wa huduma za afya pindi wanapougua na wakawa hawana fedha. Kwa takwimu za mwaka 2019/20 matumizi ya malipo ya papo kwa hapo (yaani out of pocket) kwa huduma za afya kwa kaya moja yenye watu sita yalifikia wastani wa shilingi 560,598.00 sawa na jumla ya shilingi trilioni 1.7 kwa mwaka kwa nchi nzima. Utaratibu wa malipo ya papo kwa hapo umekuwa changamoto kubwa inayosababisha wananchi wengi kutokuwa na uhakika wa kupata huduma za afya ambapo mpaka sasa asilimia 85 ya watanzania hawana bima za afya. Aidha, baadhi ya kaya zimejikuta zinaingia kwenye umaskini kutokana na kuuza mali zao ili kupata fedha za kugharamia matibabu.

Ndugu Wanahabari,

Wote ni mashahidi kuwa kumekuwana ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza ambayo matibabu yake hugharimu fedha nyingi. Mathalani gharama ya tiba ya mgonjwa wa Saratani ni shilingi milioni 26,245,000 kwa mwaka, wakati gharama ya kusafisha damu kwa mgonjwa mwenye matatizo ya figo ni shilingi milioni 32,898,000 kwa mwaka. Hivyo, kutokana na gharama kubwa za matibabu baadhi ya wananchi wanashindwa kumudu

gharama hizo na kupata athari za kiafya na wakati mwingine hata kupoteza maisha kutokana na kukosa huduma bora za afya. Katika kutatua changamoto hiyo, Serikali imedhamiria kutunga Sheria ya bima ya afya kwa wote ili kuimarisha mfumo wa bima ya afya kwa kuwezesha wananchi kuchangia gharama za matibabu kabla ya kuugua kwa kujiunga na bima ya afya na hivyo, kuwawezesha kupata huduma bora za afya wakati wote wanapozihitaji karibu na maeneo wanakoishi.

Ndugu Wananchi,

Sheria za bima ya afya zilizopo kwa sasa, hazijajumuisha makundi yote ya wananchi katika mfumo wa bima ya afya na hivyo kuacha kundi kubwa la wananchi (asilimia 85) nje ya mfumo wa Bima ya afya. Kwa mfano, hadi mwisho wa mwaka 2021, kati ya watanzania wanaokadiriwa kufikia milioni **57,724,380** ni wananchi milioni **8,567,486** sawa na asilimia 15 ya wananchi wote ndiyo wanaonufaika na mfumo wa huduma za bima ya afya. Hali hii imeendelea kuwa changamoto na kusababisha kukosekana kwa uhakika wa kupata huduma za afya kwa kundi kubwa la wananchi walio nje ya mfumo wa bima ya afya.

Ndugu Wanahabari,

Serikali ilianza hatua za awali za maandalizi ya Kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote tangu mwaka 2012. Kutokana na umuhimu na ukubwa wa suala hili, Serikali ililazimika kutumia muda mrefu katika kufanya uchambuzi wa mambo mbalimbali ili kupata namna nzuri ya kutekeleza suala hili ikiwa

ni pamoja na kushirikisha wa makundi na wadau mbalimbali katika jamii ambapo kwa sasa tayari Serikali imekamilisha mchakato huo.

Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuutaarifu umma wote wa watanzania kuwa, baadaya ya miaka 10 ya majadiliano na makundi mbalimbali, Serikali ya Awamu ya Sita (6) chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tayari imekamilisha rasimu ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya na imewasilisha rasimu ambayo imesomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Sheria ya bima ya afya kwa wote itaweka utaratibu wa kuchangia gharama za matibabu kabla ya kuugua ambapo kila mtu atapatiwa kadi baada ya kujiunga na bima ya afya, utaratibu ambao utakuwa na manufaa makubwa sana kwa wananchi.

Ndugu Wanahabari,

Utaratibu huu utawawezesha wananchi kuchangiana, ambapo anaeumwa na kuhitaji matibabu atachangiwa gharama za matibabu wale ambao watakuwa hawaumwi kwa kipindi husika. Hivyo, utaratibu huu unaondoa hali iliyopo sasa inayomlazimu mtu kubeba mzigo peke yake wa kulipa gharama kubwa za matibabu anapokuwa ameugua. Kupitia utaratibu huu, ni kawaida kwa mwananchi kulipa kiwango kidogo cha fedha kwa kujiunga na bima ya afya na akapatiwa matibabu ya gharama kubwa kuliko kiasi cha fedha alicholipia wakati najiunga na bima ya afya. Pili, utaratibu huu unampa mtu uhuru wa

kutafuta fedha na kulipia kadi ya bima ya afya bila ya kuwepo hali ya dharura kama ile ambayo mtu huwa nayo wakati anapohitaji kulipia papo kwa papo huduma za matibau anapokuwa ameugua au kuuguliwa. Hivyo, kulipia kabla ya kuugua kutawezesha kila mwananchi kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha kutokuwa na fedha na kuiwezesha Serikali kufikia lengo la Afya kwa wote (UHC)

Ndugu Wanahabari,

Wakati wa utekelezaji wa Sheria hii, wananchi watakuwa na uhuru wa kujiunga na Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya au Kampuni binafsi zinazotoa huduma ya bima kadri kila mtu atakavyoona inafaa. Aidha, kwa upande wa Serikali tumejiandaa kutekeleza Sheria ya bima ya afya kwa wote pindi itakapopitishwa na Bunge. Baadhi ya maeneo ambayo Serikali imekuwa ikijiandaa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa dawa za kutosha na vipimo vya uchunguzi wa magonjwa katika vituo vya umma vya kutolea huduma. Aidha, kwa lengo la kupata uzoefu na kuendelea kuboresha huduma zitakazotolewa kwa wananchi chini ya utaratibu huu, Serikali imepanga kutekeleza sheria hii, hatua kwa hatua kwa kuanzia na baadhi ya makundi katika jamii.

Ndugu Wanahabari,

Pamoja na kwamba kila mtu anatakiwa na Sheria hii kujiunga na bima ya afya, Serikali haikusudii kutekeleza Sheria hii kwa kukamata watu ambao kwa kipindi Fulani watakuwa hawajajiunga na bima ya afya. Aidha, katika kutekeleza ulazima huo, Serikali inatarajia kufungamanisha umiliki wa kadi ya bima ya afya na upatikanaji wa baadhi ya huduma za kijamii kama ambavyo baadhi ya huduma zilivyofungamanishwa na umiliki wa kadi au namba ya Kitambulisho cha Taifa(NIDA). Lengo la kufungamanisha umiliki wa kadi ya bima ya afya na baadhi ya huduma ni kuepuka adhabu za kukamata na kushitakiwa mahakamni kwa watu wasio na kadi ya bima ya afya kwa kuwa kufanya hivyo hakutaiwezesha Serikali kufikia lengo la kila mwananchi kupata huduma za afya. Kwa upande mwingine, kufungamanishwa kwa baadhi ya huduma za kijamii kunatarajia kuweka msukumo kwa wananchi ili wachukue hatua za kujiunga na bima ya afya ili kuepuka changamoto za kutokuwa na uhakika wa kupata huduma za afya wanapozihitaji kutokana na kikwazo cha fedha. Aidha katika kutekeleza hili, Serikali imeanza kutekeleza mpango wake wa kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa sheria ili kila mmoja awe tayari kujiunga na bima ya afya afya yake.

Ndugu Wanahabari,

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, pamoja na mambo mengine itazingatia mambo muhimu yafuatayo:

- (i) Kuweka kitita cha mafao chenye usawa ambacho kila mwananchi atakayejiunga na bima ya afya atakuwa na haki ya kukipata,
- (ii) Kutoa fursa kwa wananchi wote kupata huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma vya umma na binafsi kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Rufaa ya Taifa,
- (iii) Kuweka viwango vya michango ya bima ya afya kulingana na hali halisi ya gharama za utoaji wa huduma za afya. Kwa kuanzia, kiwango cha mchango wa kujiunga na bima ya afya ni shilingi 340,000 kwa kaya ya watu sita inayojumuisha mchangiaji, mwenza wake na wategemezi wasiozidi wanne kwa mwaka. Kiwango hicho ni sawa na wastani wa shilingi 28,400 kwa mwezi au shilingi 945 kwa siku.

Aidha, kwa wale watakaohitaji huduma za bima nje ya utaratibu wa familia (mtu mmoja mmoja) watachangia kiasi cha shilingi 84,000 kwa mwaka sawa na wastani wa shilingi 7,000 kwa mwezi au shilingi 235 kwa siku. **Vilevile wananchi watakaotambuliwa kutokuwa na uwezo wataendelea kupatiwa huduma kwa utaratibu utakaowekwa na Serikali.**

- (iv) Kuimarisha mfumo wa utambuzi wa wananchi wasio na uwezo ili kuiwezesha Serikali kuweka utaratibu madhubuti wa upatikanaji wa huduma za matibabu wakati wanapozihitaji,
- (v) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mfumo wa bima ya afya nchini ili kulinda haki na wajibu wa wadau wote katika utekelezaji wa mfumo wa bima ya afya, na
- (vi) Kutoa fursa kwa Sekta binafsi ikiwemo Kampuni Binafsi za Bima ya Afya kushiriki katika kutoa huduma za bima ya afya kwa wananchi wote.

Ndugu wanahabari,

Kama nilivyoieleza awali, Sheria ya bima ya afya kwa wote inatoa fursa kwa watu kujiunga na mfumo wa bima ya afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya au Kampuni binafsi zinazotoa huduma za bima ya afya nchini. Aidha, kwa kuzingatia ukweli kwamba, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ndiyo unaohudumia wananchi wengi (8%) kati asilimia 15.3 ya wananchi wote waliojiunga na bima ya afya kwa sasa, nimeona sina budi kutoa maelezo mafupi kuhusu Mfuko huu.

Ndugu Wanahabari

Pamoja na kuwepo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), sheria ya sasa ya kujiunga kwa hiari imesababisha changamoto nyingi. Kutokana na hali hiyo, wanachama wengi waliojiunga kwa hiari wamekuwa wakitumia matibabu yenye gharama kubwa kuliko kiwango kinachokubalika ikilinganishwa na michango wanayotoa kwa mwaka na hivyo kuwepo kwa mwenendo usio na uwiano mzuri kati ya mapato na matumizi ya Mfuko. Mathalani, Kundi la wanachama wa Toota Afya Kadi na Ushirika Afya, ni moja ya makundi ya yanayotumia zaidi ya asilimia 100 ya michango inayotolewa kwa Mfuko. Wakati wanachama kupitia kundi la Toto Afya Kadi linatumia asilimia 299 ya michango yao kwa Mfuko ambapo wanachama wa kundi la Ushirika Afya linatumia asilia 154. Hali imedhoovisha sana mfuko wa NHIF.

Ndugu Wanahabari,

Pamoja na makundi niliyoyaeleza hapo juu kutumia kiwango kikubwa cha fedha za Mfuko kwa ajili ya kugharamia matibabu, pia kumekuwepo ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo hutumia gharama kubwa kuyatibu na kwa muda mrefu. Mathalani, idadi na gharama za magonjwa yasiyoambukizwa miongoni mwa wanufaika wa Mfuko imeongezeka kutoka **bilioni 35.65** mwaka 2016/17 hadi **bilioni 101.92** mwaka 2020/21. Kwa upande mwingine, gharama ya kuwahudumia wanachama ambao wamestaafu kutoka kwenye utumishi wa umma na kuendelea kuhudumiwa na Mfuko bila kuchangia imeendelea kuongezeka kutoka Shilingi 17,968,091,847 mwaka 2016/17 hadi shilingi

60,714,576,710 mwaka 2020/21. Sababu zote hizi zimechangia sana NHIF kuyumba.

Ndugu Wanahabari,

Napenda kuwahikikishia kuwa, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, tayari imeshachukua hatua madhubuti zenye lengo la kuondoa naksi katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Afya na kuufanya kuwa imara ambapo kwa sasa upo tayari kuwahudumia wananchi wote watakachagua kujiunga na mfumo wa bima ya afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Ndugu Wanahabari,

Kabla sijamaliza taarifa yangu hii kwa umma, aomba nitumie fursa hii kutoa rai kwa wadau wakati tukijiandaa kukamilisha jambo hili muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu katika sekta ya afya kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Wananchi wote kutumia fursa hii kujiunga na bima ya afya mara baada ya bunge kupitisha Sheria hii ili kila mwananchi awe na uhakika wa kupata huduma za afya pindi anapozihitaji bila kikwazo cha fedha.
- (ii) Waajiri wote kutoka sekta binafsi na Serikali kujiandaa kutekeleza sheria hii na,
- (iii) Watoa huduma wote katika sekta ya afya ambao ni hospitali zote, kampuni na mifuko ya bima za afya kuwa tayari kutekeleza sheria hii na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Ndugu Wanahabari,

Naomba nimalizie kwa kusema, pamoja na dhamira njema ya kutunga Sheria hiyo, Serikali inatambua umuhimu wa kuwapa fursa wananchi ili waweze kutoa maoni kwa lengo la kuboresha muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kabla haijapitishwa na Bunge. Napenda kuwahakikishia wananchi kuwa fursa hiyo inaandaliwa na wananchi watajulishwa ili kutoa maoni yao wakati utakapofika. Aidha, Serikali imepanga kuzindua kampeni mahususi ya kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya na namna mpango wa bima ya afya kwa wote utakavyotekelezwa nchi nzima. Kampeni hiyo itafanyika katika Mikoa, Wilaya na Kata zote Tanzania Bara.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Imetolewa na;

Umyy A. Mwalimu (Mb)
Waziri wa Afya